**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

**WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI**

**TAARIFA KWA UMMA**

## UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA MIZANIA YA MWAKA NA HESABU ZA KAMPUNI

Dar es Salaam – 06 Agosti, 2026

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (*BRELA*) inapenda kuwakumbusha Wamiliki, Wakurugenzi na Makatibu wa Kampuni kuwa huduma ya uwasilishaji wa taarifa ya Mizania ya mwaka na hesabu za Kampuni (*Annual returns and Audited Annual Accounts*) zinatakiwa kuwasilishwa kwa msajili wa kampuni kama sheria inavyoelekeza kwa mujibu wa kifungu namba 131 cha sheria ya kampuni, sura 212 toleo la mwaka 2023.

Kampuni binafsi na za umma zinatakiwa kuwasilisha taarifa hizi kwa msajili wa kampuni kila mwaka pindi ifikapo tarehe na mwezi ambao kampuni ilisajiliwa *(Anniversary of Incorporation*) au tarehe nyingine yeyote ambayo kampuni itakuwa imechagua na kumtaarifu msajili wa kampuni nae akaridhia.

Aidha, kampuni za kigeni (*Foreign Companies*) zinatakiwa kuwasilisha hesabu za mwaka kila inapofika tarehe ya hesabu (*Accounting Date*) kama ilivyojazwa katika taarifa za kampuni BRELA.

Hivyo, kupitia mfumo ulioboreshwa wa BRELA Online System *(BOS)*, Mmiliki, Mkurugenzi au Katibu wa Kampuni atatakiwa kuwasilisha taarifa hizo kwa Msajili. Kwa mteja ambae bado ana akaunti katika mfumo wa awali wa ORS anatakiwa kutumia anuani ya barua pepe (*Email*) iliyotumika katika mfumo wa ORS, kisha kubonyeza kitufe cha '*Forget Password'*, ambapo mtumiaji atapokea ujumbe kwenye barua pepe utakayomwezesha kuingia kwenye mfumo wa BOS.

Kwa kampuni ambayo haijakidhi takwa hili haitaweza kufanya mabadiliko ya taarifa yoyote yanayoletwa kwa msajili hadi ombi la ukamilishwaji wa taarifa hizo limekamilika.

Kwa maelezo zaidi au usaidizi wa haraka, tafadhali wasiliana nasi kupitia simu +255 (0) 22 2212800 au tutumie barua pepe kupitia support.bos@brela.go.tz.

Imetolewa na;

**Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma**